**OFISI YA RAIS –TAMISEMI**

**Namba za simu (0767881048/0676598378)** **Shule ya sekondari Murusagamba**

**Mkuu wa shule: NGEZE KABILIGI JOHN** **S.L.P 334,**

**Ngara**

**…………....**

**Makamu mkuu wa shule: Laurent L. Mtoba (0765157098/0788034878)**

**Simu ya mezani: 0662718505(10:00-12:00)jioni**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi**

……………………………………………………………………………………………………

S.L.P ………………………

**YAH: <u>MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MURUSAGAMBA:</u>**
**<u>HALMASHSURI YA WILAYA YA NGARA MKOA WA KAGERA MWAKA ………:</u>**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha Tano katika shule hii mwaka ……… katika tahasusi ya PCB, CBG, HGL,HKL, HGFa na HGLi. Shule ya sekondari MURUSAGAMBA ipo umbali wa kilometa105 kutoka Ngara mjini na kilometa 30 kutoka barabara kuu inayoelekea nchini Rwanda/Burundi.

   Ukisafiri kwa basi kutoka Dar es salaam, kahama, Mwanza na mikoa mingine telemkia kituo cha mabasi cha Mizani (Nyakahura) kisha panda magari madogo kuelekea Murusagamba sekondari. Nauli kutoka Mizani mpaka Murusagamba kituoni ni Tsh.4000/= na kutoka kituoni hadi shuleni ni Tsh. 2000/=.kwa usafiri wa pikipiki.

Muhula wa masomo unaanza tarehe ………….. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ………. kwa ajili ya usajili na kuanza masomo rasmi siku ya jumatatu ya tarehe …………...

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:**

2.1 :**Sare ya shule**

(a) Sare ya shule hii ni Suruari mbili nyeusi kwa wavulana zenye marinda mawili na ziwe zimepindwa kwa chini yaani ziwe na “Turn up” na zisibane miguuni (upana miguuni sm18) modo haziruhusiwi kabisa.

(b) Shati 2 nyeupe za mikono mirefu iliyo na alama ya kidato cha tano ( V ) mabegani ya kitambaa cha suruari na tai mbili ndefu nyeusi.

(c) Sare ya michezo kwa shule hii ni viatu raba nyeupe,bukta moja ya rangi ya daki bluu na Tshirt moja ya rangi ya daki bluu yenye kola isiyo na mandishi au alama yeyote pamoja na soksi ndefu za michezo rangi ya bluu.

(d) Sare ya kushindia ni suruari moja rangi daki blue pamoja na track suit rangi ya kijivu yenye misitari myeupe na Tshirt ya rangi ya daki bluu yenye kola ambayo ina nembo ya shule, isipopatikana inaweza patikana karibu na mazingira ya shule kwa wanaoziuza.

(e) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi.
(f) Soksi jozi mbili nyeusi.

(g) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi.

(h) Jaketi zito lenye rangi nyeusi ambalo litavaliwa wakati wa usiku tu kwa ajili ya baridi na Sweta kwa ajili ya baridi (rangi zambarau ) ambapo unaweza kulivaa muda wa masomo wakati wa mchana usipoipata unaweza kuipata karibu na mazingira ya shule kwa wanaoziuza.

(i) Uje na Sanduku la chuma/Mbao kwa ajili ya kutunzia vifaa vyako.

(j) Uje na kopi ya result slip na cheti cha kuzaliwa namba ya kitambulisho cha NIDA cha mzazi wako.

(k) **Uje na kadi ya bima ya afya (NHIF) au Tsh. 50400/= kwa ajili ya kukatia Bima hiyo.**

(l) Aje na solata kwa ajili ya mwanga pindi umeme unapokatika.

(**Vifaa hivi vitakaguliwa mara utakaporipoti shuleni).**

**NB:Kumbuka nguo za kiraia ambazo sio sare za shule na ambazo hazikutajwa zisiletwe kabisa shuleni na haziruhusiwi kuvaliwa shuleni.**

**2.2 :Vifaa vya masomo**

i. Daftari 10 kubwa (counter books).

ii. Daftari 10 ndogo kwa ajili ya majaribio ya mwezi

iii. Kalamu za wino wa bluu au nyeusi.

iv. Mkebe wa hisabati (Mathematical sets)

v. Mfuko wa vitabu(school bag)

**N.B: Vifaa vyote vinapatikana karibu na mazingira ya shule (murusagamba center)**

**2.3Michango ya shule**

(a) **Michango inayotakiwa kulipwa na kila mzazi ni:-**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

Angalizo jumla ya michango ni **Tsh. 80,000/=**

**NB:Fedha taslimu (cash) hazipokelewi, badala yake fedha yote ilipwe bank kwenye account ya shule:MURUSAGAMBA SECONDARY SCHOOL , AKAUNTI NAMBA 32101200058 NMB BANK TAWI LOLOTE.njoo na bank payslip**

(b) **Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapswa kuleta shuleni**:-

i. Ream 2 za karatasi kwa mwaka au 1 kila muhula size A4 aina ya **Double A.**

ii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

iii. Dissecting kit kwa wanafunzi wa PCB na CBG.

iv. Non programmable scientific calculator kwa wanafunzi wa PCB na CBG

v. Godoro lenye saizi 2.5"X6" aje nalo.

vi. Mashuka pea 2 za rangi ya Bluu, blanketi 1,mto na foronya 1 rangi ya bluu, chandarua 1 rangi ya bluu.

vii. Vyombo vya chakula (sahani ya bati,bakuli, kijiko na kikombe)

viii. Ndoo mbili ndogo na beseni moja la kufuria ambapo ndoo moja itakabidhiwa shuleni.

ix. Jembe na mpini wake 1 , slasher 1,mopa(sponge mop) 1 ,soft broom(fagio laini 1),mfagio wa nje 1 (chelewa wenye mti),kwa **HGFa** walete **brush** ya chooni 1 badala ya **soft broom** na **HGLi** walete **kotama** 1 badala ya **soft broom** kwa ajili ya kufanyia usafi.

x. Wanafunzi wa masomo ya sanaa waje na Oxford Advanced learners Dictionary kwa kila mmoja..

NB:Ili kupunguza usumbufu wa ubebaji wa vifaa hivyo unaweza ukavipata madukani Murusagamba senta.

**Taratibu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na

uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.

iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku na alfajiri ( night and morning preparation).

iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;

v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;

ix. Kutunza mali za shule;

x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.Mawasiliano yote yatumie simu ya mezani kupitia namba **0662718505.Hata hivyo mwanafunzi ataruhusiwa kutumia simu hiyo siku za wikendi tu kuanzia saa saba mchana hadi saa kumi na mbili kamili jioni.**

Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.

Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
ii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
iv. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
v. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa a nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule.
vi. Kufuga ndevu.
vii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya.
viii. Uvutaji wa sigara.
ix. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa.
x. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xi. Kusababisha mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa.
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.
xviii. Kutii kengere.

3. **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya** wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. **TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule (0767881048/0676598378)**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0765157098**
- **Mwandamizi Taaluma 0767220903**
- **Mwandamizi Malezi 0744674378**

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

Saini ya mkuu wa shule 


Jina la Mkuu wa shule: **NGEZE KABILIGI JOHN**

ORODHA YA VITABU ZIADA

CHEMISTRY

- ABC ChemistryForHigherLevel
- RamsedChemistryForHighLevelAndCollege
- RodgersMuncasterForHighLevelAndCollege

BIOLOGY

- D.J. Taylor etal (1984): BiologicalScience2ndor3rdedition.Cambridge University press.uk
- UnderstandingBiology

PHYSICS

- A-levelPhysicsbyRogerMuncaster
- SChand.PrincipleofPhysicsforclassXIbyV.K. Mehta & Rohit Mehta
- AdvancedLevelPhysics7thEdbyNelkon & Parker

GEOGRAPHY

- ComprehensiveApproachtophysicalGeographyby D.T. Msabila
- Zist Kamili:GeographyIIArriveHumanandEconomicGeography
- GeneralinDiagramsbyR.B. Burnett
- Zist Kamili:PracticalGeography

HISTORY

- Ck Shibitali(2015,2016,2017 edition) Contemporary world Events
- D.E Butendeli (2016) Major trands in world history from medieval era to present Advanced level Compehensive notes History paper 2
- Oxford Advanced learners History form 5

KISWAHILI

- Nadharia ya lugha Kiswahili 1 kidato cha tano na sita- Nyambali Nyangwine
- Nadharia ya lugha Kiswahili 2 kidato cha tano na sita fasihi kwa ujumla
- Tahakiki ya vitabu teule kidato cha tano na sita.

GENERAL STUDIES

- Comprehensive book for Advanced level secondary schools- Mwajabu b. Mruma
- Genera studies –Nyambali Nyangwine

- General studies Alive-Zisti Kamili

ENGLISH LANGUAGE

- Advanced English Language Form 5&6 by James John (Oxford University press)

Mwanafunzi anunuliwe vitabu kulingana na tahasusi (combination) yake. Unaweza kumnunulia kimoja kwa kila somo kama hali ya uchumi hairuhusu kununua aina zote.

(FOMU HII IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI) SHULE YA SEKONDARI MURUSAGAMBA, S.L.P 334, NGARA.

KIAPO CHA MWANAFUNZI Mimi ……………………………… ……………………………………………………….

(Jina la mwanafnzi) nimezisoma sheria hizi na kuzielewa niko tayari kuzitekeleza Sahihi……………………………… tarehe……………………………….....

MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. JINA KAMILI……………………………………………………………..

(Jaza kama ilivyo kwenye selform)

2. MAJINA MATATU YA MZAZI/MLEZI..............................................................

3. ANUANI YA NYUMBANI……………………………………………………..

4. TAREHE YA KUZALIWA (mwanafunzi)……………….. MAHALI ULIPOZALIWA……………….. WILAYA……………………KATA …………………………TARAFA ………………………………

5. SHULE YA SEKONDARI ULIPOTOKA………………………ANUANI …………………………

6. DINI YAKO ……………………………..Kiwango Cha elimu Cha Mzazi,......................

UTAIFA: MTANZANIA/SI MTANZANIA (Futa lisilo sahihi)

JAMAA KATIKA FAMILIA YENU

(a) JINA LA BABA …………………………………… ANUANI ……………………………

ANAISHI/HAISHI…………………………………..NAMBA YA NIDA,......................

KAZI YAKE…………………………………………NAMBA YA SIMU……………………… (b) JINA LA MAMA……………………….........ANUANI………………………………..

(c) ANAISHI/HAISHI………………………………….. NAMBA YA NIDA ..........................

(d) KAZI YAKE…………………………………………NAMBA YA SIMU………………………

(e) JINA LA MLEZI………………….................................ANUANI…………………………………

KAZI YA MLEZI …………………………………....NAMBA YA SIMU………………………… UHUSIANO WAKE NA WEWE……………………………………………….

(f) IDADI YA KAKA ZAKO ………………………………...

(g) IDADI YA DADA ZAKE……………………………………………………………

(h) WEWE WANGAPI KATIKA FAMILIA? ..........................................................

Mimi……………………………………………………………………....(mwanafunzi) NATHIBITISHA KUWA TAARIFAZILIZOJAZWA HAPO JUU NI ZA KWELI.

(Sahihi ya mwanafunzi) …………………………………....

Mimi………………………………………(mzazi/mlezi wa mwanafunzi…………………………

NIMEHAKIKISHA KUWA TAARIFA ZILIZOJAZWA HAPO JUU NI ZA KWELI. NA NINAKIRI

KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI , KULIPA ADA, MICHANGO NA MAELEKEZO MENGINE YATAKAYOTOLEWA NA SHULE

………………………………............

………………………………………………….

(Sahihi ya mzazi/mlezi) (Tarehe)

NB: Uje na picha moja (1) passport size za wazazi na ndugu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.(moja kwa kila mmoja)

FOMU HII IJAZWE NA KURUDISHWA SHULENI SHULE YA SEKONDARI MURUSAGAMBA, S.L.P 334, NGARA.

MAHUSIANO YA MLEZI (MM)

Wazazi/walezi wanajulishwa kuwa barua yenye kuleta ujumbe muhimu kwa wanafunzi kumwombea ruhusa , aje nyumbani kwa shughuli muhimu/maalumu ni lazima iandikwe na mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni.

Kuhusu masuala mbalimbali yayomuhusu mwanafunzi shule haitakuwa tayari kujadili na mtu/ndugu yeyote anayejitokeza, bali masuala yote yamhusuyo mwanafunzi yatajadiliwa au mawasiliano yatafanyika kati ya shule na mzazi/mlezi aliyeandikishwa shuleni. Mtu mwingine hatakubalika labda kwa idhini maalumu iatakayoandikwa na mzazi/mlezi mwenyewe.

(Wahusika watakuwa ni hawa tu) walioorodheshwa hapa chini

1. JINA LA BABA……………………………………………………….(Hai/si hai) KAZI YAKE(kama yu hai) …………………NAMBA YA SIMU………………….

ANUANI…………………………………….NAMBA YA NIDA…………………………

2. JINA LA MAMA………………………………………………………..(Hai/si hai) KAZI YAKE (kama yu hai)…………………………………………………………

ANUANI …………………….NAMBA YANIDA………………………………

3. Mlezi ni Yule mtu uliyemteua kama mzazi hayupo,kukuwakilisha katika masuala ya mwanafunzi huyu.

JINA LA MLEZI……………………………………………………………… … KAZI YAKE………………………………………………………………………………..

ANUANI……… ……….……..NAMBA YA NIDA………………………

.NAMBA YA SIMU………………….

……………………………………… ……………………………………………..

(sahihiyamzazi/mlezi) (tarehe)

NB:JAZA SEHEMU ZOTE TATU KWA WATU WATATU TOFAUTI

NGARA DISTRICT COUNCIL,

MURUSAGAMBA SECONDARY SCHOOL

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

REF. No……………………………………

TO THE MEDICAL OFFICER GOVERNMENT HOSPITAL
NAME……………………………………………………………………….

AGE…………………………………….. SEX ……………………….

Please examine the above named student and arrange for any necessary treatment for the student.

MEDICAL CERTIFICATE (Tobecompletedbymedicalofficer) I have examined the above name with regards to:

REMARKS

Eyes………………………………………………………………………………………
……….

Blood……………………………………………………………………………………….
………

Abdomen…………………………………………………………………………………
………….
Pressure…………………………………………………………………………………
……………
Chest……………………………………………………………………………………
…………….

Urine
…………………………………………………………………………………………
…… TB-Test
…………………………………………………………………………………………
….

Syphilis Test
……………………………………………………………………………………….
Disabilities (if
any)……………………………………………………………………………………

Additional information:

Eg: Physical effects or important infection, chronic or family diseases etc

1. The student is now in good health out of infections

2. He/she is now fit to go/return to school after treatment for
………………………………………….

3. Please certify that above is fit to be admitted at secondary school as a student.

COMMENTS:……………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………………………………………………………………………

Doctor’s signature Designation and Official stamp

……………………….. ………………………………